MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

Taftishi Kuhusu
Tuhuma Dhidi ya Makampuni ya Mafuta Nchini Kupanga na Kupandisha bei za Mafuta Mnamo Julai 2007 kwa Minajili ya Kujipatia Faida Isiyostahili

na

Mapungufu ya Ufanisi kwenye Mfumo wa Usambazaji Bidhaa za Mafuta ya Petroli Yanayopelekea Kuazishwa kwa Udhibiti Uchumi[1]

(INQ-P-07-001)

AGIZO Na. 07-010

Mnamo mwezi Julai 2007 kulikuwepo na kile kilichoonekana kuwa ni ongezeko lisilokubalika la bei za bidhaa za mafuta ya petroli nchini kufuatia kupandishwa kwa kodi kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/08. Mwezi Agosti 2007, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilirekebisha Sheria ya Kuhifadhi Mafuta ya Petroli Sura ya 392 (Petroleum Conservation Act) na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Sura ya 414 (EWURA Act), ili kuipa EWURA mamlaka ya kudhibiti masuala ya kiuchumi kwenye sekta ya mafuta, (yaani uagizaji, uuzaji na usambazaji). Kufuatia marekebisho hayo, EWURA imepewa mamlaka, pale itakapoona inafaa, ya kuingilia kati na kudhibiti mwenendo wa kiuchumi kwa lengo la kupunguza wigo wa maamuzi kuhusu upangaji wa bei, kiwango cha faida kwenye mtaji, na katika kuchagua mfumo wa manunuzi ya bidhaa za mafuta ya petroli.

EWURA ilifanya Taftishi kuchunguza chanzo cha kupanda kwa bei za mafuta mwezi Jalai 2007, ikiwa ni pamoja na kupata taratibu za namna EWURA itakavyodhibiti masuala ya kiuchumi kwenye sekta ya mafuta. Kama sehemu ya Taftishi, wito ulitolewa kwa wadau wote kupitia vyombo vya habari ili wawasilishe maoni na taarifa juu ya masuala hayo. Aidha, kwenye mkutano wa Taftishi uliyofanyika kwenye ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam tarehe 31 Agosti 2007, EWURA ilipokea na kujadili maoni mbalimbali kutoka kwa wadau. Katika mkutano wa Taftishi hiyo, mada mbalimbali ziliwasilishwa. Pia, baada ya mkutano, michango mingine ya maandishi kutoka kwa wadau iliwasilishwa EWURA.

[1] Tathmini ya kina kuhusu Taftishi hii inapatikana katika tovuti ya EWURA ambayo ni www.ewura.com

Kufuatia kukamilika kwa Taftishi hiyo, EWURA imebaini yafuatayo:

(i) Tuhuma Dhidi ya Makapuni ya Mafuta ya Kupanga na Kupandisha Bei

Imeshindikana kupata ushahidi unaothibitisha kuwepo kwa upangaji wa bei wa pamoja kati ya makampuni ya mafuta. Hata hivyo, nadharia za kiuchumi zinaonyesha kwamba katika mazingira yenye ushindani, kampuni yenye hisa kubwa katika soko huanza kupandisha bei na kufuatiwa na makampuni mengine. Hivyo, ongezeko la bei kwa mara moja na kwa makampuni yote lilikuwa ni tukio lisilo la kawaida.

(ii) Makampuni ya Mafuta Kujipatia Faida Isiyostahili

Uwiano kati ya ongezeko la kodi na kupanda kwa bei ya mafuta mwezi Julai 2007 unaonyesha kuwa wakati kodi ilipanda kwa Shilingi 124 kwa lita ya petroli, Shilingi 122 kwa lita ya dizeli, na Shilingi 0 kwa lita ya mafuta ya taa, **wastani** wa ongezeko la bei katika vituo vya mafuta ulikuwa Shilingi 135 kwa lita ya petroli (yaani shilingi 11.10 zaidi ya ongezeko la kodi), Shilingi 35.47 kwa lita ya dizeli (yaani Shilingi 86.53 chini ya ongezeko la kodi), na bei ya mafuta ya taa ilipungua kwa **wastani** wa Shilingi 31.56 kwa lita.

Ongezeko kubwa (zaidi ya ongezeko la kodi) katika bei ya petroli ilipekelea umma kuamini kwamba makampuni ya mafuta yalijipatia faida isiyostahili.

(iii) Mapungufu ya Ufanisi Kwenye Mfumo wa Usambazaji Bidhaa za Mafuta ya Petroli

Taftishi ilibaini mapungufu yafuatayo katika mfumo wa usambazaji wa bidhaa za mafuta ya petroli:

(a) utaratibu wa kila kampuni kuagiza mafuta yake kutoka nje unasababisha gharama kubwa za usafiri; msongamano wa meli

bandarini na hivyo kusababisha ada za ucheleweshaji wa meli; pamoja na kuhamisha gharama za makampuni mama kwa watumiaji;

(b) malipo na ada mbalimbali zinazotozwa kwenye mafuta yanayoagizwa nchini kwa ajili ya huduma zinazotolewa na taasisi mbalimbali nchini yanaongeza mzigo wa bei kwa mnunuzi. Ada hizo hutozwa kwa misingi ya ama thamani ya shehena ya mafuta, viwango thabiti (fixed rates), au kwa kuzingatia ujazo wa shehena. Aidha, baadhi ya taasisi hutoza ada hizo kwa kutumia viwango vya fedha za kigeni na wengine fedha ya Tanzania. Ada hizi huchangia katika mabadiliko ya mara kwa mara ya bei za bidhaa za mafuta ya petroli;

(c) kuna haja ya kuangalia upya utaratibu wa upatikanaji na ukodishaji wa huduma ya kuhifadhi mafuta katika matanki makubwa;

(d) kukithiri kwa uuzwaji wa bidhaa za mafuta ya petroli zisizo na ubora katika vituo vingi vya mafuta hapa nchini. Hali hiyo husababisha athari za kiafya, ukwepaji kodi, uharibifu wa magari na mitambo na kusababisha mazingira ya biashara yasiyo sawa kiushindani, hasara kwa watumiaji huduma na Serikali kukosa mapato;

(e) vituo vingi vya mafuta vimejengwa bila kuzingatia taratibu na viwango vinavyokubalika hivyo kuhatarisha afya, usalama wa mali na uharibifu wa mazingira; na

(f) baadhi ya vituo vya petroli havionyeshi bei za bidhaa zake.

Katika kuhitimisha tafitishi hiyo, EWURA ilibainisha kuwa sekta ya mafuta ya petroli ina mapungufu na kwamba uamuzi wa Serikali wa kuipa EWURA mamlaka ya kudhibiti masuala ya kiuchumi kwenye sekta hiyo umekuja wakati muafaka. Sekta hii imetawaliwa na kasoro mbalimbali ikiwemo uagizaji wa shehena ndogo ndogo za mafuta, ukwepaji kodi, kukosekana kwa taarifa muhimu na uchanganyaji wa mafuta (adulturation).

Katika kikao chake cha tarehe 8 Oktoba 2007, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ilitafakari masuala haya na kufanya maamuzi yafuatayo:

1. Makampuni yote ya mafuta yanayoingiza bidhaa za mafuta nchini, yataagiza bidhaa zao za mafuta kwa utaratibu wa pamoja (Bulk Importation System) kwa uwazi na kwa kutoa zabuni zenye ushindani wa kimataifa.

2. Kwa kushirikiana na taasisi husika, EWURA itafanya tathmini ya ada mbalimbali zinazotozwa na taasisi zinazotoa huduma kwa waagizaji wa mafuta nchini.

3. Makampuni ya mafuta yanayomiliki miundombinu ya kuhifadhia mafuta yatalazimika kutangaza masharti na ada za matumizi ya miundombinu hiyo. Masharti na ada hizo zitapitiwa na kuidhinishwa na EWURA kabla ya kuanza kutumika.

4. Vituo vyote vya mafuta vitalazimika kuandika na kuweka mahali pa wazi bei wanazotoza kwa kila bidhaa ya mafuta ya petroli.

5. Wauzaji wote katika vituo vya petroli watalazimika kununua bidhaa za mafuta kutoka kwa wasambazaji wenye leseni za usambazaji mafuta ya petroli.

6. Waagizaji na wenye vituo vya mafuta ya petroli waliopo sasa wanatakiwa kuomba leseni husika kabla ya tarehe 31 Desemba 2007. Mwombaji yeyote kati yao atakayewasilisha maombi yake baada ya tarehe 31 Desemba 2007 atatozwa ada ya kuchelewa ya Shilingi 1,000,000/=.

7. Kuanzia tarehe 1 Novemba 2007, EWURA itakuwa inatangaza mlinganisho wa bei za bidhaa za mafuta ya petroli na kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei kwenye vituo vya petroli kwa minajili ya kuleta ushindani katika soko. Taarifa hii inatolewa kuwasaidia watumiaji kufanya maamuzi kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta ya petroli.

Simon F. Sayore
Mwenyekiti wa Bodi

Haruna Masebu
Mkurugenzi Mkuu

Dar es Salaam, 8 Oktoba 2007